



Kindy katika Queensland

Kindy ni nini?

Shule ya chekechea, inayojulikana kuwa kindy, ni programu ya kielimu ya muda kwa watoto katika mwaka kabla ya Prep (mwaka wa kwanza wa shule katika Queensland). Kindy ni mahali ambapo mtoto wako atajifunza kupitia Uzoefu ya mchezo na mahusiano ambao yanaunga mkono ujifunzaji wao wa mapema, ustawi na ukuaji.

Kwa kushiriki katika kindy, watoto wanajifunza kupenda kujifunza na wanaungwa mkono na mda wa mapito wao kwenda Prep.

Programu za kindy zinazoidhinishwa na Serikali ya Queensland zinatolewa na mwalimu mwenye hitamu wa utoto wa mapema. Programu za Kindy zinaweza kutolewa katika vituo vya elimu ya watoto wa mapema; shule zilizoachaguliwa za vijijini na mbali na shule nyingine zilizoachaguliwa ambapo kulikuwa na vizuizi kuingia chekechea; na kwa elimu ya mbali au Kindy ya mtandaoni (eKindy) kwa watoto wengine wasioweza kufikia kituo.

Kujifunza kwenye kindy

Kindy hutoa fursa kwa watoto wadogo:

- kutumia lugha ili kuwasiliano mawazo, hisia na mahitaji
- kupata marafiki, kuwasiliana na kushirikiana na wengine
- kutambua masuala na kupata ustadi wa kutatua matatizo
- kuweza kujiamini zaidi na kuweza kujitegemea katika ustadi wao
- kuungana na, kuchunguza na kuchangia katika mazingira yao
- kujenga ujuzi na kuchunguza mawazo mapya, kusaidia kujenga kujiamini zaidi.

Je,umesikia?

Free **KiNDY** from 2024

Free
KiNDY



Queensland
Government

Jinsi ya kujiandikisha

Katika Queensland, watoto wanaweza kuhudhuria kindy katika mwaka kabla ya kuanza Shule ya Mwanzo (Prep).

Kila huduma ni tofauti na baadhi ya huduma huenda kuwa na orodha ya kungoja, kwa hiyo ni wazo zuri kuzungumza na huduma unayochagua kuhusu wakati mzuri wa kujiandikisha mtoto wako.

Mtoto wako lazima awe na umri wa miaka 4 kabla ya tarehe ya 30 Juni katika mwaka ambao anajiandikisha kushiriki katika kindy.

Mtoto alizaliwa	Mtoto anaweza kuhudhuria kindy
1 Julai 2019 hadi 30 Juni 2020	2024
1 Julai 2020 hadi 30 Juni 2021	2025
1 Julai 2021 hadi 30 Juni 2022	2026
1 Julai 2022 hadi 30 Juni 2023	2027
1 Julai 2023 hadi 30 Juni 2024	2028
1 Julai 2024 hadi 30 Juni 2025	2029

Kitu unachohitaji ili kumuandikisha mtoto wako:

- jina na anwani ya mtoto wako
- maelezo yako kama mzazi wake, mtunzaji au mlezi
- maelezo ya maagizo yoyote ya mahakamani au maagizo au mipango ya uzazi
- maelezo ya msaada wowote wa ziada unaohitajika (k.m. ulemavu, chakula, mzio au mahitaji mengine)
- uthibitisho wa tarehe ya kuzaliwa (k.m. cheti cha kuzaliwa)
- hali ya afya na ya kuchanjwa
- maelezo ya watu wanaoruhusiwa kumkuta mtoto wako na kumjulisha nani katika hali ya dhurura.

Huduma yako atatunza taarifa hii kuwa siri na utakuwa na upatikanaji mzima kwa rekodi za mtoto wako.

Uliza mtoaji wa kindy ya eneo lako kuhusu

Free
KINDY
from 2024

Kuchagua programu ya kindy

Watoto wote wa Queensland wanastahiki kuhudhuria programu ya kindergarten katika mwaka kabla ya kuanza Prep.

Program iliyoidhinishwa ya shule ya chekechea inatosheleza miongozo ya serikali, na:

- ni programu ya kujifunza inayotolewa na walimu wenye sifa kwa watoto wa mapema, kulingana na miongozo ya serikali.
- hutolewa kwa masaa 15 kwa wiki, wiki 40 kwa mwaka, kwa watoto ambao wamo mwaka kabla ya Prep
- inalingana na mwongozo wa ujifunzaji wa chule ya chekechea ya Queensland au programu nyingine ya ujifunzaji iliyoidhinishwa ya Mamlaka ya Mtaala na Tathmini ya Queensland.

Ili kusaidia kupata programu inayoidhinishwa na Serikali ya Queensland, tafuta kwa 'alama ya idhini ya kindy', yaani picha hapa chini.



Queensland
Government

Kindy ya Bure kuanzia mwaka 2024

Serikali ya Queensland inafanya shule kuwa bure kwa familia zote za Queensland.

Kindy itakuwa bure kwa watoto wenye umri wa kustahiki wanaohudhuria programu iliyoidhinishwa na serikali ikitoa kindy ya bure kutoka tarehe ya 1 Januari 2024.

Hii ni masaa 15 kwa wiki, wiki 40 kwa mwaka, ya kindy ya bure inayofundishwa na mwalimu mwenye sifa wa utoto wa mapema.

Familia zinaweza kuchagua kindy katika chule ya chekechea ya vipindi au shule ya chekechea iliyomo kituo cha matunzo ya siku ndefu.

Ili kupata kindy ya bure ya karibu sana kwako, tembelea:
www.qld.gov.au/FreeKindy